TANGAZO LA SERIKALI Na. 50Q la tarehe. 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA MAPATO YA KAMPUNI KATIKA MRADI WA UANZISHAJI WA SHAMBA LA MIWA, UKAMUAJI WA MIWA NA UFUNGASHAJI WA SUKARI KWA KAMPUNI YA M/S MUFINDI PAPER MILLS YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Mapato ya Kampuni katika Mradi wa Uanzishaji wa Shamba la Miwa, Ukamuaji wa Miwa na Ufungashaji wa Sukari kwa Kampuni ya M/S Mufindi Papers Mills ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 3 Julai, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya mapato ya kampuni katika Mradi wa Uanzishaji wa Shamba la Miwa, Kusimika Mtambo wa Ukamuaji wa Miwa na Ufungashaji wa Sukari inayopaswa kulipwa na Kampuni ya M/S Mufindi Papers Mills Limited inasamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafikia ukomo wake tarehe 31 Mei, 2028 kwa kuzingatia kifungu cha 3.4 cha mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya M/S Mufindi Papers Mills Limited na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*